

MUHTASARI

- Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua, wakulima wanaendelea na shughuli za palizi isipokuwa baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Shinyanga ambapo msimu wa mvua umechelewa kuanza.
- Msimu wa mvua umeanza kwa maeneo ya Kigoma, Rukwa na Tabora na wakulima wameanza kupanda mazao.
- Kutokana na hali ya ukavu wa muda mrefu kwa maeneo mengi ya Shinyanga, Dodoma, Singida, Longido na Kiteto, wafugaji wanashauriwa kutumia malisho na maji kwa uangalifu.


**MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA
KIPINDI CHA NOVEMBA 11-20, 2017**

Katika kipindi tajwa, migandamizo ya hewa iliyo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kupungua nguvu wakati migandamizo iliyo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) iliendelea kuimarika, hivyo kuruhusu ukanda wa mvua (ITCZ) kuelekea kusini mwa dunia. Joto la bahari katika bahari ya Hindi liliendela kuwa juu kidogo ya wastani na kusababisha maeneo ya pwani kuwa na vipindi vya mvua. Kwa upande mwingine joto la bahari la juu ya wastani liliendelea kuongezeka katika eneo la Kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) hali iliyosababisha kupunguza kwa mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi na ukanda wa Ziwa Viktoria.

**MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI
CHA NOVEMBA 11-20, 2017**

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa iliyokuwepo, maeneo mengi ya katika mikoa ya Tabora, Mara, Geita, Shinyanga, na baadhi ya maeneo ya Kigoma, Rukwa, Mbeya, Mtwara, Morogoro, Tanga na Pwani yalipata mvua pungufu kwa milimita (mm) 20 hadi 50 chini ya wastani wa muda mrefu katika kipindi cha siku 10 husika (angalia Kielelezo Na. 1). Pia, upungufu mkubwa zaidi (hadi 100 mm chini ya wastani) ulionekana katika maeneo machache ya mikoa ya Mara, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro na mashariki mwa mkoa wa Lindi. Hata hivyo mvua za zaidi ya 100 mm

zilinyesha katika maeneo machache ya mkoa wa Lindi, Manyara na kisiwa cha Pemba kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na. 1.



Kielelezo Na. 1. Mwenendo wa mvua katika kipindi cha Tarehe 11-20 Novemba, 2017.

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 11-20, 2017

Hali ya unyevu wa udongo ilikuwa chini ya wastani katika maeneo mengi nchini. Hata hivyo, wakulima waliopanda mapema wameendelea na palizi hususan katika maeneo ya kanda ya ziwa Viktoria, pwani ya kaskazini na ukanda wa pwani ya kaskazini isipokuwa mkoa wa Shinyanga ambapo msimu wa vuli umechelewa kuanza. Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kama mkoa wa Tabora, Rukwa na Kigoma msimu wa mvua umeanza na wameshaanza kupanda mazao. Maeneo yaliyosalia wakulima wanaendelea na maandalizi ya mashamba kwa ajili ya msimu unaotarajiwa kuanza wiki ya nne ya Novemba hadi Disemba 2017. Katika kipindi cha siku kumi hizo, upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo ulikuwa wa wastani katika maeneo mengi ya nchi kutokana na mvua za *Vuli* zinazoendelea kunyesha, isipokuwa katika baadhi ya maeneo ya Simiyu, Shinyanga, Dodoma, Singida, Longido na Kiteto ambako hali ya maji na malisho bado si ya kuridhisha.

HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 11-20, 2017

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito vimeanza kuongezeka hususan maeneo yanayopata misimu miwili wa mvua kutokana na mvua za vuli zinazoendelea.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2017

Migandamizo ya hewa iliyo kusini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu wakati, ile iliyopo sehemu za kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika na hivyo kuruhusu ukanda wa mvua wa ITCZ kuelekea sehemu ya kusini mwa dunia. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi na hii inaweza kusababisha mvua katika maeneo ya ukanda wote wa pwani. Kusini-magharibi mwa bahari ya Atlantiki kunatarajiwa kuendelea kuwepo kwa joto la juu ya wastani na hivyo kupunguza mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi na Ukanda wa Ziwa Viktoria.

HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2017

Maeneo ya **Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu)**: Vipindi vya mvua vitakavyoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache. **Nyanda za juu kaskazini-magharibi (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara)**: Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache. **Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba)**: Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora)**: Vipindi vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida)**: Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache. **Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Njombe, Iringa na Mbeya)**: Vipindi vya mvua vitakavyo ambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi)**: Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma)**: Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2017

Mvua zinazotarajiwa zitaongeza unyevunyevu kwenye udongo kwa ajili ya mazao na malisho. Wakulima wanashauriwa kuzitumia mvua hizi kwa shughuli za kilimo. Kwa maeneo ambayo mvua za msimu hazijaanza kunyesha wakulima wanashauriwa kuendelea kuandaa mashamba. Wakulima na wafugaji wanashauriwa kufuata ushauri wa maafisa ugani na kuchukua hatua stahiki. Pia wafugaji wanashauriwa kutumia malisho na maji kwa uangalifu.

HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA NOVEMBA 21-30, 2017

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa mito kinatarajiwa kuongezeka katika maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka hususan bonde la maji la Ziwa Viktoria, Pangani na Wami/Ruvu. Watumiaji wa maji wanashauriwa kuyatumia kwa uangalifu.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania